



“UPIMAJI NA UNASIHI”

Upimaji na unasihi vina nafasi kubwa sana katika uzuiaji wa VVU kwa kuwasaidia watu kuhimili ugonjwa na kuepuka kuwaambukiza watu wengine. Lakini:

- Chini ya asilimia 10 ya watu wa Afrika wanajua hali yao ya maambukizi ya VVU.
- Huduma za upimaji na unasihi zinapatikana kwa asilimia 24 tu ya watu wa Afrika.
- Mara nyingi wanasihhi wanakosa mafunzo au muda, hivyo kusababisha huduma kuwa mbaya.
- Hofu, kukataliwa, unyanyapaa, na ubaguzi vyote huasababisha watu washindwe kuitumia huduma hiyo inapatikana.

Utafiti miongoni mwa vijana walio katika umri wa balehe na vijana wengine katika nchi nyingi umeonyesha kuwa hawakuwa tayari kupima iwapo huduma hizo haziwahakikishii mazingira mazuri.

- Baadhi ya vijana nchini Swaziland wametoa taarifa ya kutembea mbali kutoka nyumbani kwao ili kupimwa katika kituo cha afya ambako wao na familia zao hawana mtu wanaemfahamu. Wengi wao hawawezi kuvumilia hali hiyo.
- Nchini Ghana, vijana wamelalamika kuwa kwenda kupimwa kumesababisha fedheha kwao na familia zao na hudhaniwa kuwa “waasherati” au wana UKIMWI.

Katika nchi nyingi, watu wenye VVU hivi sasa wanaweza pia kupata matibabu yatakayowaruhusu kuendelea kuishi na kupata nafuu kwa miaka mingi.

Programu ya Masa au Mapambazuko mapya nchini Botswana imeongeza idadi ya watu wanaojua hali yao ya VVU kwa kufanya kupima kuwe sehemu ya matibabu yao. Hii ni habari njema kwa nchi ambazo viwango vya kuenea kwa VVU miongoni mwa watu wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 49 ambao ni asilimia 35 (katika jumla ya watu 1.7 milioni).

- Katika Programu ya Masa (Mapambazuko mapya) kupima si lazima ingawa huduma hii inatolewa kwa anayependa, (kwahiari) madaktari wanasema kuwa ni watu wachache sana wanaokataa kuitumia.
- Baada ya miaka miwili ya programu, zaidi ya theluthi moja ya watu wanajua hadhi yao ya VVU. Hii ni mara tatu ya sehemu ya watu wanaojua hali yao ya VVU katika nchi nyingi za Afrika:
- Jambo jingine linalotia moyo ni kwamba, idadi ya wanawake wanaohudhuria kliniki ya wajawazito waliogunduliwa na VVU imepungua kwa asilimia 15 kati ya mwanzoni mwa mwaka 2004, wakati programu ilipoanza na mwishoni mwa mwaka 2005.
- Wanaharakati wa UKIMWI nchini Botswana wanaamini kwamba watu wengi zaidi wanakubali kupima kwa sababu ya matumaini yanayotokana na matibabu mbalimbali yaliyopo, na kudhihirisha uhusiano wa karibu kati ya kupima, matibabu na kinga/uzuiaji.



TAARIFA HALISI NAMBA NNE



Kupunguza au kuondoa gharama za upimaji kunaweza pia kuwa na athari kubwa, kama ilivyoonyeshwa katika matokeo ya programu ya upimaji ya kiwango kidogo katika kliniki zilizopo nchini Tanzania.

- Wakati upimaji wa VVU ulitolewa bure na idadi ya watu waliojitolea kupima iliongezeka kutoka wastani wa watu 4 hadi 15 kwa siku.
- Wakati ada/gharama ndogo (sawa na dola moja ya Marekani) ilipowekwa, idadi ya watu imepungua kwa nusu.
- Wakati programu ya kupima bure ilipoanzishwa tena, idadi ya watu iliongezeka tena kutoka 15 hadi 18 kwa siku.
- Ongezeko la watu limefanya kupimwa kusiwe na gharama kubwa. Kila kipimo kiligharimu **dola 170** za Marekani wakati walipopimwa watu **wanne kwa siku**. Gharama ya kipimo **ilipungua hadi dola 92** za Marekani wakati **watu 15 walipopimwa kwa siku**.

Mafunzo kwa watoa huduma ni muhimu sana ili kuhakikisha kuwa wanao uwezo wa kutoa ushauri unaofaa kulingana na mahitaji ya kila mteja. Kwa wanawake wajawazito, kwa mfano, taarifa kuhusu uamuzi wa kujifungua na kulisha mtoto mchanga ni muhimu kwa kuzuia maambukizi ya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Kwa sasa, upungufu wa wauguzi na wanasihhi wenye mafunzo unaathiri sana ubora wa unasihhi katika nchi nyingi (**angalia makala ya Tano**).

Hitimisho

Kupima kunakojumuisha huduma za kupima na unasihhi wa hiari (VCT), pamoja na upimaji wa kawaida, kuna nafasi muhimu sana katika kuzuia maambukizi ya VVU, lakini kuongeza idadi ya watu na huduma ya upimaji kunakabiliwa na vikwazo mbalimbali katika nchi nyingi za Afrika, kama vile:

- Gharama za upimaji.
- unyanyapaa unaoambatana na kupima.
- Upungufu wa wafanyakazi wenye uelewa na mafunzo ya kutosha wanaoweza kunasihhi kwa usahihi watu wazima na vijana.
- Huduma duni za matibabu na hivyo kupunguza hamasa/ari ya kupima.

Kupanua upimaji pamoja na VCT, kutahitaji:

- Kuongeza fedha katika mifumo ya mafunzo ya afya na malipo ya wafanyakazi.
- Kubadili mitazamo kuhusu wanaoishi na VVU na UKIMWI.
- Kujenga mazoea ya kupima.
- Kupanua fursa za vipimo na matibabu ya bure.